



JAMHURI YA
MUUNGANO
WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

AJENDA 10/30
KILIMO NI BIASHARA

MWONGOZO WA UZALISHAJI MAZAO KULINGANA NA KANDA ZA KILIMO ZA KIIKOLOJIA



Yaliyomo

YALIYOMO	i
VIFUPISHO	ii
DIBAJI	iii
SHUKRANI	iv
MUHTASARI	v
UTANGULIZI	vi
UMUHIMU WA MWONGOZO	1
MAZAO YA KIPAUMBELE KWA KILA KANDA	1
Kanda ya Kati	2
Kanda ya Ziwa.....	3
Kanda ya Kaskazini	4
Kanda ya Mashariki	5
Kanda ya Magharibi.....	6
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini	7
Kanda ya Kusini	8
MAZAO YANAYOFAA KUZALISHWA KIMKOA NA KIWILAYA.....	9
MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA KILIMO BORA CHENYE TIJA	30
KALENDA YA UZALISHAJI WA BAADHI YA MAZAO NCHINI	34

Vifupisho

ASDP II	Agricultural Sector Development Program Phase II
CAN	Mbolea aina ya Calcium of Ammonia
DAP	Mbolea aina ya Di Ammonium Phosphate
GDP	Pato la Taifa (Gross Domestic Product)
M	Mita (metre) Kipimo cha Urefu
MM	Milimita (Kipimo cha urefu)
NPK	Mbolea aina ya Nitrogen Phosphrous Potassium
pH	Chachu ya Udongo
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
SA	Mbolea aina ya Sulphate of Ammonia
TSP	Mbolea aina ya Triple Super Phosphate

Dibaji



Sekta ya Kilimo ni mhimili wa uchumi wa nchi na inachangia pato la mkulima mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla. Sekta hii kwa mwaka 2020 imechangia asilimia 26.9 kwenye Pato la Taifa, imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 61.1 na imechangia asilimia 65 ya upatikanaji wa malighafi za viwanda. Aidha, sekta ndogo ya mazao imechangia asilimia 15.4 katika Pato la Taifa na zaidi ya asilimia 100 ya upatikanaji wa chakula kinachozalishwa nchini. Vilevile uzalishaji wa mazao hupunguza mfumuko wa bei kwa takriban asilimia 59.

Pamoja na kujitosheleza kwa chakula na kuchangia katika uchumi wa taifa, takriban mazao yote yanazalishwa kwa tija ndogo katika eneo husika. Aidha, uzalishaji umekuwa ukipanda na kushuka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo baadhi ya mazao hayo kuzalishwa katika ikolojia isiyostahiki. Uzalishaji wa mazao nje ya ikolojia yake ya asili hupelekea kuwa na tija ndogo na wakati mwingine kuzalisha mazo kwa gharama kubwa.

Ili kuongeza uzalishaji na tija Wizara ya Kilimo imeandaa Mwongozo wa Uzalishaji Mazao Kulingana na Kanda za Kilimo za Kiikolojia. Mwongozo huu umezingatia matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika nchini kuhusu aina za udongo, hali ya hewa, mtawanyiko wa mvua na aina za mazao yanayofaa kuzalishwa kwa kila kanda. Aidha, mwongozo umeandaliwa ili kuelekeza wawekezaji na wakulima kuchagua zao linaloweza kuzalishwa kwa tija kulingana na hali ya ikolojia husika.

Ni rai yangu kuwa wadau wote nchini zikiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, taasisi za Serikali na Sekta binafsi hususan wakulima kutumia Mwongozo huu katika kuwekeza na kuzalisha mazao kulingana na mahitaji ya ikolojia. Aidha, mwongozo huu utumike sambamba na miongozo mingine ya kanuni za kilimo bora kwa mazao mbalimbali.

HUSSEIN M. BASHE (Mb)
WAZIRI WA KILIMO
MACHI, 2022

Shukrani



Nchi yetu ina Kanda Kuu Saba (7) za Utafiti wa Kilimo zenye zaidi ya Ikolojia 64 za uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ya aina mbalimbali. Kanda hizo ni Kanda ya Kati, Ziwa, Kaskazini, Mashariki, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kusini. Ili kuzalisha mazao kwa tija na kwa gharama nafuu, Wizara ya Kilimo imeandaa Mwongozo wa Uzalishaji Mazao Kulingana na Kanda za Kilimo za Kiikolojia.

Mwongozo huu ukitumiwa vizuri na wadau mbalimbali wakiwemo wakulima utawezesha Wizara kufikia lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo nchini ili kuwa na kilimo cha kisasa, chenye faida na ushindani kibiashara kwa lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi, usalama wa chakula na lishe.

Ninawashukuru wadau wote walioshiriki katika kuandaa mwongozo huu ambao ni dira katika kuongeza uzalishaji na tija katika maeneo yote kwa lengo la kukuza uchumi na pato la taifa kwa ujumla. Shukrani za dhati kwa Maafisa kutoka Idara za Sera na Mipango, Maendeleo ya Mazao, Mafunzo Huduma za Ugani na Utafiti, Kitengo cha Mazingira, MVIWATA, Chuo Kikuu Cha Kilimo Sokoine (SUA) na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) kwa kufanya kazi bila kuchoka na kukamilisha mwongozo huu. Aidha, ninaishukuru Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo (TARI) kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa za utafiti wa uzalishaji wa mazao kulingana na ikolojia ambazo zimewezesha maandalizi ya mwongozo huu.

ANDREW W. MASSAWE
KATIBU MKUU
MACHI, 2022

Muhtasari

Kulingana na taarifa za Kituo cha Utafiti wa Udongo cha Mlingano (TARI-Mlingano) Tanzania ina jumla ya Kanda kuu saba (7) za Kiutafiti wa Kilimo na Kanda ndogo 64 za kiikolojia zinazoonyesha aina ya mazao yanayoweza kuzalishwa. Kanda kuu hizo ni Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati, Kanda ya Kusini, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa.

Pamoja na Tanzania kuwa na Kanda Kuu saba (7) za Utafiti wa Kilimo na kanda ndogo 64 za Kiikolojia, kwa muda mrefu tija katika uzalishaji wa mazao hayo imekuwa ndogo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa mazao kutozingatia kanda hizo za kilimo za kiikolojia. Aidha, gharama za uzalishaji wa mazao nje ya ikolojia yake ni kubwa hususan wakati miundombinu ya umwagiliaji maji inapohitajika.

Mwongozo huu utasaidia kufikia azma ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda kwa kuwa mazao yatazalishwa kulingana na ikolojia na hivyo kutoa malighafi ya mazao kwa viwanda vinavyojengwa nchini. Uwepo wa viwanda hivyo utaongeza kasi ya uwekezaji katika kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa na kwa gharama nafuu. Mwongozo umeainisha ni wapi na ni zao gani linastahili kuzalishwa. Kwa mfano, maeneo yanayopata mvua chache yatumika kwa kuzalisha mazao yanayostahimili ukame kama vile Mtama, Muhogo, Viazi vitamu na mazao ya jamii ya mikunde (mbaazi na kunde).

Ili mwongozo utumike kikamilifu, pia kalenda ya kilimo imeandaliwa kwa kuzingatia mwenendo wa mvua katika mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa kuwa kumekuwepo na mabadiliko ya tabianchi kilimo kinachohimili mabadiliko hayo kinahamasishwa, pia wadau katika sekta ya kilimo wanashauriwa kuwasiliana na watafiti na wataalam wa kilimo walioko katika maeneo yao. Serikali itaendelea kuhimiza huduma za ugani zitolewe kwa kuzingatia mwongozo.

Mamlaka za Mikoa na Wilaya zinashauriwa kutunga sheria ndogo katika maeneo yao na kubuni njia bora za kutumia mwongozo huu. Wizara itaendelea kutoa maelekezo pale yanapohitajika ili kuhakikisha lengo la mwongozo huu linafikiwa. Mwongozo huu pia unapatikana katika tovuti ya Wizara www.kilimo.go.tz.

Utangulizi

Sekta ya Kilimo inayojumuisha Mazao, Mifugo na Uvuvi ni mhimili wa uchumi wa Tanzania kwa kuchangia katika Pato la Taifa na kutoa ajira kwa zaidi ya asilimia 61.1 ya nguvu kazi inayotumika nchini. Sekta hii pia huchangia na kujitosheleza kwa asilimia 100 ya chakula kinachozalishwa. Serikali inafanya juhudi kubwa ili mchango wa sekta hii kukue kwa zaidi ya asilimia 10 na kuwa na uhakika wa usalama wa chakula na kupunguza umaskini.

Mazao jamii ya wanga yanayozalishwa nchini ni mahindi, muhogo, mpunga na mtama, ndizi, viazi vitamu na mviringo, ngano, ulezi na uwele. Mazao Makuu ya biashara ni korosho, miwa, pamba, mkonge, tumbaku, pareto, kahawa na chai. Mazao mengine yanayozalishwa ni ya jamii ya mafuta hususan alizeti, ufuta, mawese, karanga na mbegu za pamba. Kundi la mazao mbalimbali ya bustani ni pamoja na matunda, mbogamboga, maua na vikolezo (*spices*). Kundi jingine ni mazao jamii ya mikunde yenye protini na hurutubisha udongo kutokana na uwezo wake wa kutengeneza virutubisho vya nitrojeni kutoka hewani (*nitrogen fixation*). Tanzania ina hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo cha mazao, kwa wastani hekta milioni 10.8 tu sawa na asilimia 24 ndizo zinazolimwa kila mwaka.



UMUHIMU WA MWONGOZO

Baadhi ya mazao huzalishwa nje ya mfumo wake wa kiikolojia hali inayosababisha kuwa na uzalishaji na tija ndogo. Hivyo, mwongozo huu umeandaliwa ili kuelekeza namna bora ya kuzalisha mazao ya kilimo kulingana na ikolojia. Jedwali Namba 4 hadi 10 yanaonesha hali ya sasa ya uzalishaji mazao ikilinganishwa na tija inayoweza kufikiwa endapo kanuni bora za kilimo zitazingatiwa katika ikolojia husika. Aidha, mwongozo huu unaonyesha mazao yanayofaa kuzalishwa katika Kanda (Mikoa na Wilaya), Kanuni za kilimo bora na kalenda ya mazao mbalimbali.

MAZAO YA KIPAUMBELE KWA KILA KANDA

Mazao hustawi vema na kwa tija katika kanda kulingana na hali ya hewa ya sehemu husika, mwongozo huu unaainisha mazao stahiki katika kila kanda.

Kanda ya Kati

Mazao yanayofaa kulimwa katika Kanda ya Kati katika mikoa ya Dodoma na Singida (**Jedwali Na. 1**).

Jedwali Na. 1: Mazao na wastani wa mavuno Kanda ya Kati

Na.	Zao	Hali ya uzalishaji (Tani/Hekta)		Maoni
		Uzalishaji uliopo	Lengo linaloweza kufikiwa	
1.	Alizeti	1.20	4.00	
2.	Karanga	0.93	4.50	
3.	Ufuta	0.85	3.00	
4.	Mahindi	0.89	4.00	Kipaumbele kwenye baadhi ya maeneo.
5.	Mpunga	1.25	5.00	Kipaumbele kwenye baadhi ya maeneo.
6.	Mtama	0.99	5.00	
7.	Uwele	0.87	3.00	
8.	Ulezi	1.19	4.00	
9.	Muhogo	3.88	60.00	
10.	Viazi vitamu	2.50	20.00	

Mazao ya Chakula: Mtama, Uwele, Ulezi, Muhogo na Viazi vitamu



Uwele



Mhogo



Mtama

Mazao ya Biashara: Zabibu, Alizeti, Karanga, na Ufuta



Alizeti



Ufuta



Zabibu

Kanda ya Ziwa

Mazao yanayoshauriwa kulimwa katika kanda ya Ziwa katika mikoa ya Geita, Kagera, Mara Mwanza, Shinyanga na Simiyu (Jedwali Na. 2).

Jedwali Na.2: Mazao na wastani wa mavuno Kanda ya Ziwa

Na.	Zao	Hali ya uzalishaji (Tani/Hekta)		Maoni
		Hali iliyopo	Uwezekano wa uzalishaji	
1.	Mpunga	3.10	6.00	
2.	Ndizi	4.79	35.00	
3.	Dengu	0.88	2.00	
4.	Mahindi	1.38	4.00	Hustawi zaidi Kagera & Mara
5.	Pamba	0.60	4.00	
6.	Mtama	1.28	3.00	
7.	Mbaazi	1.18	2.50	
8.	Muhogo	5.77	60.00	
9.	Viazi vitamu	4.42	20.00	

Mazao ya Chakula: Mpunga, Maharage, Ndizi, Mahindi, Mtama, Muhogo na Viazi vitamu



Ndizi



Viazi Vitamu



Mtama

Mazao ya Biashara: Pamba, Kahawa, Chai, Miwa, Dengu na Mbaazi.



Pamba



Chai



Kahawa

Kanda ya Kaskazini

Mazao yanayofaa kulimwa katika Kanda ya Kaskazini katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara (Jedwali Na. 3).

Jedwali Na. 3: Mazo na wastani wa mavuno Kanda ya Kaskazini

Na.	Zao	Hali ya Uzalishaji (Tani/Hekta)		Maoni
		Hali iliyopo	Hali iliyopo	
1.	Ngano	1.43	5.00	
2.	Shayiri	1.49	3.00	
3.	Alizeti	1.27	4.00	
4.	Mahindi	1.39	6.00	
5.	Kahawa	0.32	2.50	
7.	Mbaazi	0.93	2.50	
8.	Mpunga	3.23	6.00	
9.	Ndizi	7.34	35.00	

Mazao ya Chakula: Mahindi, Mpunga, Ndizi, Mtama, Maharage na Mazao ya bustani.



Ndizi



Ngano



Nyanya

Mazao ya Biashara: Kahawa, Ngano, Shayiri, Alizeti, Mbaazi na Maua.



Kahawa



Maua



Mbaazi

Kanda ya Mashariki

Mazao yanayofaa kulimwa Kanda ya Mashariki katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es salaam na Tanga (Jedwali Na.4)

Jedwali Na. 4: Mazao na wastani wa mavuno Kanda ya Mashariki

Na.	Zao	Hali ya Uzalishaji (Tani/Hekta)		Maoni
		Hali iliyopo	Hali iliyopo	
1.	Mpunga	1.71	6.00	Iwe kipaumbele
2.	Ufuta	1.49	2.50	Iwe kipaumbele
3.	Alizeti	1.21	4.00	Iwe kipaumbele
4.	Mahindi	1.14	6.00	Iwe kipaumbele
5.	Muhogo	6.48	60.00	Iwe kipaumbele
6.	Viazi vitamu	5.23	20.00	Iwe kipaumbele

Mazao ya Chakula: Muhogo, Magimbi, Viazi vitamu, Mpunga, Mahindi, Mazao ya mbegu za mafuta.



Mpunga



Muhogo




Alizeti

Mazao ya Biashara: Mkonge, Korosho, Miwa, Nazi, Mazao ya bustani (Machungwa, Embe, mboga mboga, viungo na vikolezo).



Mkonge



Nazi



Vitunguu swaumu

Kanda ya Magharibi

Mazao yanayofaa kulimwa katika Kanda ya Magharibi katika mikoa ya Tabora na Kigoma (Jedwali Na. 5).

Jedwali Na. 5: Mazo na wastani wa mavuno Kanda ya Magharibi

Na.	Zao	Hali ya uzalishaji - Tija (Tani/Hekta)		Mapendekezo
		Ya sasa	Uwezekano (Potential)	
1.	Muhogo	5.74	60.00	Iwe kipaumbele
2.	Ndizi	5.92	35.00	Iwe kipaumbele
3.	Mpunga	2.60	5.00	Iwe kipaumbele
4.	Mahindi	1.38	6.00	Iwe kipaumbele
5.	Karanga	0.99	4.50	Iwe kipaumbele
6.	Mbaazi	0.79	2.50	Iwe kipaumbele
7.	Kahawa	0.39	2.50	Iwe kipaumbele
9.	Pamba	0.47	4.00	Iwe kipaumbele
10.	Tumbaku	1.26	3.50	Iwe kipaumbele
11.	Viazi vitamu	4.88	20.00	Iwe kipaumbele

Mazao ya Chakula: Mahindi, Muhogo, Viazi vitamu, Ndizi, Mikunde na Mpunga



Mahindi



Muhogo



Ndizi

Mazao ya Biashara: Kahawa, Tumbaku, Michikichi, Pamba na Tangawizi



Tumbaku



Michikichi



Pamba

Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

Mazao yanayofaa kulimwa katika Kanda ya Nyanda za juu Kusini katika Mikoa ya Iringa, Katavi, Mbeya, Njombe, Rukwa, Ruvuma na Songwe (Jedwali Na. 6)

Jedwali Na. 6: Mazao na wastani wa mavuno Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

Na.	Zao	Hali ya uzalishaji - Tija (Tani/Hekta)		Mapendekezo
		Ya Sasa	Uwezekano (Potential)	
1.	Muhogo	5.96	60.00	Iwe kipaumbele
2.	Viazi mviringo	7.29	30.00	Iwe kipaumbele
3.	Mpunga	2.73	5.00	Iwe kipaumbele
4.	Mahindi	1.76	6.00	Iwe kipaumbele
5.	Ngano	0.81	5.00	Iwe kipaumbele
6.	Alizeti	1.50	4.00	Iwe kipaumbele
7.	Tumbaku	0.92	3.50	Iwe kipaumbele

Mazao ya Chakula: Mahindi, Mpunga, Maharage, Ngano, Viazi mviringo, Muhogo na Mazao ya bustani



Maharage



Viazi mviringo



Mpunga

Mazao ya Biashara: Chai, Kahawa, Tumbaku, Pareto, Alizeti, Maua



Chai



Alizeti

Kanda ya Kusini


Mazao yanayofaa kulimwa Kanda ya kusini katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Wilaya ya Tunduru (Jedwali Na. 7)

Jedwali Na. 7: Mazao na wastani wa mavuno Kanda ya Kusini

Na.	Zao	Hali ya uzalishaji – Tija (Tani/Hekta)		Mapendekezo
		Ya Sasa	Uwezekano (Potential)	
1.	Muhogo	5.25	60.00	Iwe kipaumbele
2.	Mbaazi	0.97	2.50	Iwe kipaumbele
3.	Mpunga	1.30	5.00	Iwe kipaumbele
4.	Ufuta	1.20	2.50	Iwe kipaumbele
5.	Alizeti	1.00	4.00	Iwe kipaumbele
6.	Karanga	1.35	4.50	Iwe kipaumbele
7.	Korosho	8kg/mti	30kg/mti	Iwe kipaumbele

Mwongozo huu umeainisha mazao yafuatayo kuzalishwa katika kanda hii ya Kusini:-

i. **Mazao ya Chakula:** Muhogo, Mazao ya jamii ya kunde na



Muhogo




Soya



Mbaazi


ii. **Mazao ya Biashara:** Korosho, Nazi, Ufuta, Alizeti Karanga na Mazao ya bustani



Korosho



Ufuta



Nazi

MAZAO YANAYOFAA KUZALISHWA KIMKOA NA KIWILAYA

Kila zao huhitaji mazingira maalum yanayoweza zao husika kuzalishwa kwa tija kubwa na kwa gharama nafuu. Hata hivyo, mazingira ya asili yanaweza kuboreshwa ili kustawisha mazao ambayo kwa asili yasingeweza kuzalishwa kwa tija katika maeneo hayo (Jedwali 8).

Jedwali Na. 8: Mazao yanayofaa kuzalisha katika mikoa kulingana na ikolojia

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
1	ARUSHA	Arusha	Kahawa, Maua	Mahindi, Maharage, ndizi na viazi mviringo	Mwinuko: 500 - 1,700 Mvua: 800-1,200 Joto:15-30 Udongo: pH 5-8.5. Tifutifu, kichanga na madini ya calcium, mfinyanzi na rutuba ya kutosha.	Mazao ya Bustani, alizeti, ufuta	Mikunde
		Karatu	Kahawa, Shayiri, Vitunguu maji	Mahindi, maharage,	Mwinuko: 900 - 2,500 Mvua: 200 - 1,400 Joto: 10 - 30 Udongo: pH 4 -8.5. Tifutifu, mfinyanzi, calcium na rutuba ya wastani.	Ngano na Mazao ya bustani	Mikunde
		Longido	Ndizi, Vitunguu saumu,	Mahindi, Maharage, mtama	Mwinuko:500-1,700 Mvua 400 -1,300 Joto:10-30 Udongo: pH 6.5 - 8.5. Tifutifu kichanga, mfinyanzi, madini ya chokaa (calcium) mengi na rutuba ya kutosha	Vitunguu maji, Ngano	Mikunde
		Monduli	Kahawa, Ndizi, Vitungu saumu, Mazao ya Bustani.	Mahindi, mbaazi	Mwinuko: 500-2,500 Mvua: 200-1,400 Joto:5-30 Udongo: pH 5 ->8.5. Tifutifu, kichanga na mfinyanzi, calcium nyingi na rutuba hafifu	Vitunguu maji	Viazi vitamu
		Ngorongoro	Mazao ya bustani	Mahindi, Mtama	Mwinuko: 900-2,500 Mvua: 400-1,400 Joto: 5-30 Udongo: pH 4.5-8.5. Tifutifu, kichanga madini ya calcium na rutuba ndogo	Vitunguuu saumu	Viazi vitamu

Na.	Mkoa	Wilaya	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
2	DAR ES SALAAM	Ilala	Tikiti maji, Muhogo	Muhogo, viazi vitamu	Mwinuko:0-500 Mvua: 800-1,200 Joto:25-35 Udongo:pH5-7 Kichanga, chumvi, Tifutifu na Mfinyanzi	Mchicha	Mikunde, Nazi
		Kinondoni	Tikiti maji, Maembe	Muhogo	Mwinuko:0-500 Mvua: 800-1,200 Joto:25-35 Udongo:pH5-7 Kichanga, chumvi, Tifutifu na Mfinyanzi	Matango, Mchicha	Kunde
		Temeke	Tikiti maji, maembe	Muhogo	Mwinuko:0-500 Mvua: 800-1,200 Joto:25-35 Udongo:pH5-7 Kichanga, chumvi, Tifutifu na Mfinyanzi	Matango, Mchicha, Papai	Kunde, Viazi Vitamu
3	DODOMA	Bahi	Zabibu, Mpunga	Mtama, uwele,	Mwinuko: 500 -1,400 Mvua:400 - 800	Alizeti na karanga	Mpunga, Viazi,
		Chamwino	Zabibu, Ufuta	Mtama, njugu mawe,	Mwinuko: 500 -1,400 Mvua: 400 - 800 Udongo: mwekundu na kichanga	Alizeti, karanga	Mpunga, Viazi vitamu,
		Chemba	Alizeti, Ufuta	Mtama, muhogo	Mwinuko: 500 -1,400 Mvua:400 - 800 mm	Alizeti, karanga	viazi vitamu
		Dodoma	Zabibu	Mtama, uwele, muhogo	Mwinuko: 500 -1,400 Mvua: 400 - 800	Alizeti, karanga	Mahindi, viazi vitamu, kunde
		Kondoa	Alizeti, ufuta na mbaazi	Mtama, Mahindi, muhogo	Mwinuko: 500 -1,400 Mvua: 400 - 800 Joto: 15 - 30 Udongo: Kichanga, tifutifu na mwekundu	Ufuta, karanga,	Mahindi, v/ vitamu kunde
		Mpwapwa	Alizeti, karanga	Mtama, njugu mawe,	Mwinuko: 500 -2300 Mvua:200 - 1,000 Joto:10-30 Udongo: Rutuba ya wastani	Ufuta, karanga	Mahindi, viazi, muhogo kunde

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Kongwa	Alizeti, karanga	Mtama, njugu mawe, muhogo	Mwinuko: 500 -2300 Mvua: 800 - 1000 Joto:15-30 Udongo: Tifutifu, kichanga, mfinyanzi na rutuba ya wastani	Mahindi	Mbaazi kunde
4.	GEITA	Bukombe	Pamba	Mahindi, Muhogo	Mwinuko: 900 -1,700 Mvua: 600 - 1,200 Joto:10-30 Udongo:pH 4 - 8.5 Kichanga, Tifutifu, changarawe, mfinyanzi	Mikunde, Karanga,tumbaku.	Viazi vitamu
		Chato	Pamba	Mahindi, Muhogo	Mwinuko: 1,100 -1,800 Mvua: 600 - 1,400 Joto:10-30 Udongo: Tifitifu, kichanga na rutuba kidogo	Mikunde	Viazi vitamu
		Geita	Pamba, mpunga	Mahindi, Muhogo	Mwinuko: 1,200 -1,300 Mvua: 600 - 1,400 Joto:15-30 Udongo: Kichanga, mfinyanzi, tifutifu na changarawe.	Mikunde, Nanasi.	Viazi vitamu
		Mbogwe	Pamba	Mahindi, Muhogo	Mwinuko: 1,200 -1,300 Mvua: 600 - 1,400 Joto:10-30 Udongo: Mweusi, Tifutifu, mfinyanzi na changarawe	Mikunde	Viazi vitamu
		Nyang'hwale	Pamba	Mahindi, Muhogo	Mwinuko: 1,200 -1,300 Mvua: 600 - 1,400 Joto: 10-30 Udongo: Meusi, Tifutifu, kichanga na rutuba kidogo	Mikunde	Viazi vitamu
5.	IRINGA	Iringa	Alizeti, Vitunguu Nyanya	Mahindi, Maharage,	Mwinuko: 400 -2,300 Mvua: 200 - 1,600 Joto: 5 - 27 Udongo: Kichanga, Tifutifu, Mfinyanzi	Alizeti, mpunga	Viazi mviringo
		Kilolo	Chai, Pareto	Mahindi, Maharage Viazi Mviringo	Mwinuko: 400 -2,300 Mvua: 600 - 1,600 Joto: 2 - 30 Udongo: pH 4-7, Tifutifu, mfinyanzi	Kahawa, shairi, mazao ya bustani	Ngano, Soya

Na.	Mkoa	Wilaya	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Mufindi	Chai, pareto	Mahindi, Maharage	Mwinuko: 400 -2,300 Mvua: 600 - 1,600 Joto: 5 - 25 Udongo: pH 4-7, Tifutifu, mfinyanzi	Alizeti, Mazao ya bustani	Viazi mviringo
6	KAGERA	Biharamulo	Kahawa, Ndizi	Ndizi, mikunde, muhogo, na mahindi.	Mwinuko: 1100 -1,800 Mvua: 600 - 1,400 Joto:10-30 Udongo: pH 4 - 7 Mchanganyiko, tifutifu, kichanga, mfinyanzi.	Alizeti na Mazao ya bustani.	viazi vitamu, viazi vikuu, magimbi.
		Bukoba	Kahawa, Ndizi, Vanila na chai.	Ndizi, mikunde na mahindi.	Mwinuko: 1200 -1,800 Mvua: 800 - 1,400 Joto:10-30 Udongo: pH 4 - 7 Mchanganyiko, tifutifu, kichanga, changarawe, mfinyanzi	Alizeti, mpunga, mazao ya bustani	viazi vitamu, viazi vikuu, magimbi
		Karagwe	Kahawa.	Ndizi, mikunde na mahindi.	Mwinuko: 1200 -1,800 Mvua: 800 - 1,200 Joto:10-30 Udongo: pH 4-7 Mchanganyiko, tifutifu, kichanga, changarawe, mfinyanzi	Alizeti, mpunga, mazao ya bustani na vanilla	Viazi vitamu, vikuu
		Kyerwa	Kahawa.	Mahindi, Ndizi na mpunga.	Mwinuko: 1,200 -1,800 Mvua: 800 - 1,200 Joto:10-30 Udongo:pH 4-7 Mchanganyiko, tifutifu, kichanga, changarawe, mfinyanzi.	Vanilla, chai Alizeti, mazao ya bustani	viazi vitamu, magimbi na muhogo.
		Misenyi	Kahawa, Vanila na Miwa	Ndizi, mikunde na Mahindi	Mwinuko: 1,200 - 1,800 Mvua: 800 - 1,400 Joto:10-30 Udongo:pH 4 -7 Mchanganyiko, tifutifu, kichanga, changarawe, mfinyanzi	Pamba, mazao ya bustani.	viazi vitamu, magimbi na muhogo.

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Muleba	Kahawa, Chai	Ndizi, mikunde na Mahindi.	Mwinuko: 1200 - 1,600 Mvua: 800 - 1,400 Joto:10-30 Udongo: pH 4-7 Mchanganyiko, tifutifu, kichanga, changarawe, mfinyanzi	Pamba, Chai, mazao ya bustani, Vanila	viazi vitamu, magimbi muhogo na njugumawe.
		Ngara	Kahawa, Pamba	Ndizi, mikunde, muhogona Mahindi	Mwinuko: 1300 -1,800 Mvua: 800 - 1,200 Joto: 10-30 Udongo. pH 4 - 7 Mchanganyiko, Tifutifu, kichanga, changarawe na mfinyanzi	Pamba, Chai, mazao ya bustani.	Viazi vitamu, magimbi, mtama na muhogo.
7.	KATAVI	Mlele	Tumbaku, Karanga, ufuta	Mpunga, Viazi vitamu, mahindi, maharage, muhogo	Mwinuko: 800-2,200 Mvua: 1,000-1,400 Joto 15-30 Udongo: pH 6 - 8, tifutifu, kichanga na rutuba kidogo	Pamba, alizeti, ulezi	Karanga
		Tanganyika	Tumbaku, Ufuta	Mpunga, Viazi vitamu	Mwinuko: 800-2,200 Mvua: 1,000 -1,400 Joto: 15-30 Udongo: pH5-7 tifutifu, kichanga na rutuba kidogo	Mazao ya bustani	Karanga
		Mpanda	Tumbaku, mchikichi	Mpunga, Viazi vitamu, mahindi, maharage	Mwinuko: 900 - 2,300 Mvua: 600-1,400 Joto: 10-15; PH 5-7 Udongo: pH 5 - 8.5 Tifutifu, kichanga na rutuba kidogo	Mazao ya bustani, ulezi	Karanga
		Mpimbwe	Tumbaku, alizeti, ufuta	Mpunga, viazi vitamu	Mwinuko: 900 - 2,300 Mvua: 600-1,400 Joto: 10-15 PH 5-7 Udongo: pH 5 - 8.5 Tifutifu, kichanga na rutuba kidogo	Mazao ya bustani	Karanga

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
8.	KIGOMA	Buhigwe	Kahawa, Tangawizi, Ndizi.	Muhogo, Mikunde, Mahindi	Mwinuko: 1,000-1,700 Mvua: 1,000-1,200 Joto: 18 - 30 Udongo: pH 5 - 7 Mchanganyiko, tifutifu, kichanga, changarawe, mfinyanzi wenye rutuba ndogo	Michikichi, Mazao ya bustani, Alizeti	Viazi mviringo
		Kakonko	Tumbaku, Michikichi, Kahawa	Mtama, Mikunde na Ndizi Mpunga	Mwinuko: 900-1.600 Mvua: 600-1,200 Joto:18-30 Udongo: pH 5-7 Tifutifu, kichanga, rutuba kubwa, mfinyanzi	Mazao ya Bustani, Kahawa na Alizeti Soya	Muhogo na Mahindi
		Kasulu	Kahawa, Michikichi, Tangawizi, Tumbaku	Mahindi, Mikunde, Ndizi na Muhogo	Mwinuko: 800-1,200 Mvua: 600-1,000 Joto:18-30 Udongo: pH 5-7 Tifutifu, kichanga, rutuba kubwa, mfinyanzi, mchanganyiko mwekundu	Mazao ya bustani, Miwa, na Alizeti	Mpunga
		Kibondo	Pamba, Kahawa, Tumbaku Michikichi.	Mahindi, Mikunde	Mwinuko: 800-1,200 Mvua: 600-1,000 Joto:18-30. Udongo: pH 5-7, Mchanganyiko mwekundu, tifutifu, kichanga, changarawe, mfinyanzi.	Mazao ya bustani na Kahawa	Ndizi, Muhogo na Mtama
		Kigoma	Michikichi na Kahawa	Mahindi, maharage, Muhogo na Mikunde	Mwinuko: 800 -1,800 Mvua: 600 - 1,200 Joto:18-30 Udongo: pH 5-7 Tifutifu, kichanga, rutuba kubwa, mfinyanzi wenye rutuba tofauti tofauti	Mazao ya bustani, Mpunga	Karanga, Ndizi na Viazi vitamu
		Uvinza	Tumbaku, Michikichi, Mpunga	Mahindi, Muhogo na Mikunde	Mwinuko: 800-1,500 Mvua: 600-1,200 Joto:18-30 Udongo:pH 5-7 Mchanganyiko mwekundu, tifutifu, kichanga, mfinyanzi wenye rutuba tofauti tofauti (chini, wastani na juu)	Mazao ya bustani, ufuta, Miwa	Ndizi na Viazi vitamu

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
9	KILIMA NJARO	Hai	Kahawa, mazao ya bustani, Mbaazi	Mahindi, Maharage, Ndizi	Mwinuko: 500-3,500 Mvua: 800-1,400 Joto: 15-30 Udongo: pH 5-8.5 Udongo wa volcano, kichanga, tifutifu, mfinyanzi, changarawe na rutuba ya wastani	Ndizi, mikunde	Mtama, viazi mviringo na vitamu
		Moshi	Kahawa, Mazao ya bustani, Parachich, mpunga, miwa	Ndizi, Mahindi, Maharage	Mwinuko: 500-3,500 Mvua: 400-1,200 Joto: 5-31 Udongo: pH 5->8.5 Mchanganyiko, tifutifu, mfinyanzi, changarawe na wenye rutuba ya asili ya wastani	Ndizi, mikunde	Mtama, viazi mviringo na vitamu
		Mwanga	Tangawizi, Fiwi, Mpunga	Mahindi, Magimbi,	Mwinuko: 500-2,000 Mvua: 400-1,000; Joto: 10-30 Udongo:pH 4.5->8.5 kichanga, tifutifu, mfinyanzi na rutuba kidogo	Kahawa, miwa	Ndizi, viazi mviringo
		Rombo	Kahawa	Ndizi, Mahindi, Maharage	Mwinuko: 500-3,500 Mvua: 400-1,200 Joto: 5-30 Udongo: pH 5-8.5 Udongo wa volcano, kichanga, Mfinyanzi, tifutifu na rutuba ya wastani	Kahawa, ulezi, ndizi	Mtama, viazi mviringo, mhogo
		Same	Tangawizi, Fiwi	Mtama, uhogo, Viazi vitamu.	Mwinuko: 500-2,000 Mvua: 400-1,000 Joto: 10-31 Udongo: pH 4.5->8.5, mchanganyiko wa kichanga na tifutifu, mfinyanzi, miamba na rutuba hafifu.	Mazao ya bustani	Ndizi, mtama
		Siha	Ngano, Kahawa, maua, viazi mviringo, mbaazi	Mahindi, Ndizi, Maharage	Mwinuko: 500-3,500 Mvua: 800-1,400 Joto: 15-30 Udongo: pH 6.5-8.5 volcano, kichanga, tifutifu, mfinyanzi, changarawe na rutuba ya wastani	Kahawa, Mikunde Mazao ya bustani	Maharage, mtama

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
10	LINDI	Kilwa	Ufuta, Korosoho, Nazi	Muhogo, mpunga, mtama	Mwinuko: 200-750 Mvua: 800-1,200 Joto: 20-28 Udongo: pH 5.5-7 Tifutifu, mchanga, Mfinyanzi	Machungwa, Tikiti maji, Maembe	Magimbi, Mpunga
		Lindi	Ufuta, Korosho	Muhogo, Mtama, Kunde	Mwinuko: 200-750 Mvua: 800-1,200 Joto: 20-28 Udongo: pH 5.5-7 Tifutifu na mfinyanzi	Nazi, Tikiti maji	Magimbi
		Liwale	Ufuta, Korosho	Mhogo, Mtama, Viazi vitamu	Mwinuko: 200-1,000 Mvua: 800-1,200 Joto: 24-28 Udongo: pH 5.5-7 Tifutifu, kichanga	Karanga	Mtama, mahindi
		Naching wea	Ufuta, Korosho, Karanga	Mhogo, Mtama, Viazi vitamu	Mwinuko: 200-1,000 Mvua: 800-1,000 Joto: 20-28 Udongo: pH 5.5-7 Tifutifu, mchanga, Mfinyanzi na Changarawe.	Karanga, Soya, Alzeti, njugu mawe	Mikunde, Maharage Mahindi
		Ruangwa	Ufuta, korosho, nazi	Mhogo, kunde na mbaazi	Mwinuko: 200-1,000 Mvua: 800-1,000 Joto: 20-28 Udongo: pH 5.5-7 Tifutifu, mchanga, Mfinyanzi na Changarawe.	Alizeti, Mazao ya bustani	Mahindi na mikunde
11	MANYA RA	Babati	Mbaazi, Alizeti	Mahindi, Mpunga, maharage	Mwinuko: 1,000-2,500 Mvua: 200-1,400 Joto: 15 - 28 Udongo: Tifutifu, mfinyanzi	Karanga, ufuta, miwa	Ndizi
		Hanang	Ngano, Mbaazi, shahiri	Mahindi, Mikunde, maharage	Mwinuko: 1,100 -2,500 Mvua: 200-700 Joto: 15 - 28 Udongo: Tifutifu, mfinyanzi	Vitunguu saumu	Viazi mviringo, Ndizi

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Kiteto	Mahindi, mbaazi	Mahindi, Maharage	Mwinuko: 700 -1,200 Mvua: 400-1,000 Udongo: pH 5-7, rutuba nyngi, tifutifu	Alizeti, soya	Viazi mviringo, ndizi, mtama
		Mbulu	Mbaazi, ngano, shahiri	Mahindi na Maharage	Mwinuko: 1,200-2,300 Joto: 10 - 28 Udongo: Tifutifu, mfinyanzi	Ngano, Vitunguu saumu	Viazi mviringo, ndizi
		Simanjiro	Ufuta, Alizeti, mbaazi	Mahindi, maharage, mtama	Mvua: 600-1,200 Joto: 15 - 28 Udongo: Tifutifu, mfinyanzi,	Ngano, mazao ya bustani	Mtama, uwele
12	MARA	Bunda	Pamba, mpunga	Mtama, Muhogo	Mwinuko: 1,000- 1,800 Mvua: 400-1,000 Joto: 10-30 Udongo:pH 6.5-8.5 Mchanganyiko, kichanga, tifutifu, mfinyanzi mweusi	Mpunga, Mazao ya bustani	Mahindi, viazi vitamu
		Butiama	Pamba	Mahindi, Mtama, ulezi	Mwinuko: 1,000-1,800 Mvua: 400-1,000 Joto: 15-30 Udongo:pH 6.5-8.5 Mchanganyiko, tifutifu, mfinyanzi mweusi	Mikunde	Viazi vitamu, Mhogo
		Musoma	Pamba, mpunga	Mtama, ulezi, Muhogo	Mwinuko: 1,000-1,200 Mvua: 600-1,400 Joto: 15-30 Udongo:pH 6.5-8.5 Mchanganyiko, kichanga, tifutifu, mfinyanzi, wenye rutuba hafifu.	Mikunde, karanga	Viazi vitamu, mahindi
		Rorya	Pamba	Mtama, Mhogo	Mwinuko: 1,000-2,300 Mvua: 500-1,200 Joto: 10-30 Udongo: pH 5-7,Mchanganyiko, kichanga, tifutifu, mfinyanzi mweusi	Mazao ya bustani	Viazi vitamu

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Serengeti	Pamba, ufuta, tumbaku	Muhogo, Mtama, mahindi	Mwinuko: 1,000- 2,300 Mvua: 500-1,200 Joto: 15-30 Udongo:pH 6.5->8.5 kichanga, tifutifu, Mfinyanzi mweusi na rutuba kiasi	Tumbaku, ufuta, mahindi	Viazi vitamu
		Tarime	Chai, kahawa, alizeti	Muhogo, Mtama, ndizi	Mwinuko: 1,000- 2,300 Mvua: 800-1,600 Joto: 10-27 Udongo:pH 4-7, Mchanganyiko, tifutifu, mfinyanzi, rutuba kiasi	Viazi mviringo, Mazao ya bustani	Mahindi, Viazi vitamu,
13	MBEYA	Busekelo	Chai, kakao, mpunga, mazao ya bustani	Mahindi, Maharage, Viazi Mviringo, ulezi	Mwinuko: 500-2,400 Mvua: 1,000-2,400 Joto 15 - 25 Udongo: ph 4-7, mfinyanzi, tifutifu na kichanga	Ndizi, Mazao ya bustani, njegere	Ndizi
		Chunya	Tumbaku, Alizeti	Mpunga, Mahindi	Mwinuko: 800-1,800 Mvua: 200-1,400 Joto 15 - 30 OC, Udongo: pH 5-7 mchanganyiko kichanga na mfinyanzi, changarawe	Ufuta, Matunda	Mtama, uwele
		Kyela	Kakao, kahawa, mchikichi, mpunga	Mpunga, Ndizi, mihogo	Mwinuko: 500-2,400 Mvua: 1,000-2,400 Joto 10-30, Udongo: pH 5- 7.5 mfinyanzi, tifutifu na kichanga	Matunda, Maharage	Magimbi, dengu
		Mbarali	Mpunga, alizeti, Ufuta	Mpunga, Mikunde, mahingi	Mwinuko: 800-1,500 Mvua: 200 -1,400 Joto: 15-30 Udongo:- pH 5-7 kichanga, mfinyanzi mweusi na tifutifu	Alizeti, Mazao ya bustani	Mtama, Viazi Vitamu
		Mbeya	Kahawa, Viazi Mviringo, mazao ya bustani,	Mahindi, Mpunga, Maharage, Ndizi	Mwinuko: 800-2,700 Mvua: 600-2,000 Joto 5-20 Udongo: ph 5-7, volcano, mfinyanzi, kichanga na tifutifu	Mazao ya bustani, ngano shairi	Maharage, viazi mviringo Magimbi

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Rungwe	Chai, parachichi, kahawa, maharage,	Mahindi, ndizi, maharage njerege na ulezi	Mwinuko: 500-2,400 Mvua: 1,000-2,400 Joto 5-30, Udongo: pH 4-7 volcano, udongo mfinyanzi, tifutifu na kichanga	Kokoa, ndizi, mazao ya bustani	Maharage, viazi mviringo, magimbi
14.	MORO-GORO	Gairo	Mahindi, Alizeti, Maharage	Mahindi, Viazi vitamu	Mwinuko: 400-2,300 Mvua: 800-1,600; Joto:15-30 Udongo:pH 5-7 Tifutifu na kichanga	Mikunde, Alizeti	Mpunga, mtama
		Ifakara	Mpunga, Miwa	Mpunga, Mahindi	Mwinuko: 400-2,300 Mvua: 800-1,600 Joto:20-35 Udongo: pH4-7 Tifutifu, kichanga na mfinyanzi na wenye rutuba.	Kakao, Mikunde, ufuta	Ndizi, mhogo
		Kilombero	Miwa, Mpunga, Kakao	Mpunga, Mikunde	Mwinuko: 400-2,300 Mvua: 800-1,600 Joto:20-35 Udongo: pH4-7 Tifutifu, kichanga na mfinyanzi na wenye rutuba.	Viungo/spices, Ndizi	Muhogo, Mahindi
		Kilosa	Mkonge, Mpunga, Korosho	Mahindi, Mikunde	Mwinuko: 200-2,300 Mvua: 800-1,600; Joto:15-30 Udongo: pH4-7 Tifutifu, kichanga na mfinyanzi mweusi na wenye rutuba.	Mazao-bustani, korosho, pamba	Muhogo
		Malinyi	Mpunga, Korosho	Mpunga, Mahindi	Mwinuko: 200-2,300 Mvua: 800-1,600 Joto:20-35 Udongo: pH 4-7 Tifutifu, kichanga na mfinyanzi na wenye rutuba.	Kakao, pamba, Mazao ya bustani	Mahindi, Ndizi
		Morogoro	Mkonge, Miwa, Mazao ya bustani, Viungo	Mihogo, Mahindi na mikunde	Mwinuko: 200-2,300 Mvua: 800-1,600 Joto:20-35 Udongo: pH 4-7 Tifutifu, mfinyanzi na wenye rutuba kiasi	Alizeti, Ufuta	Ndizi,
		Mvomero	Mpunga, Ufuta, Mazao bustani	Mahindi, Viazi vitamu, maharage	Mwinuko: 200-2,300 Mvua: 800-1,600 Joto:20-35; Udongo: pH4-7 mfinyanzi mweusi na rutuba kiasi	Korosho, Ufuta	Mtama, Mahindi

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Ulanga	Mpunga, Korosho	Mpunga, mahindi, maharage	Mwinuko: 200-2,300 Mvua: 800-1,600 Joto:20-35 Udongo: pH 4-7 Tifutifu, kichanga na mfinyanzi na wenye rutuba.	Ufuta, alizeti	Mahindi, mtama
15	MTWARA	Masasi	Korosho, Ufuta	Muhogo na mbaazi,	Mwinuko: 200-500 Mvua: 800-1,000 Joto:12-35 Udongo: Ph 5-7 tifutifu, kichanga na mfinyanzi	Ufuta, mazao ya bustani, soya	Mpunga
		Mtwara	Korosho, Ufuta	Muhogo, mpunga	Mwinuko: 0-300 Mvua: 800-1,000 Joto:12-35 Udongo: pH 5-7 tifutifu, kichanga na mfinyanzi	Ufuta , mazao ya bustani	Mahindi, mikunde
		Nanyamba	Korosho, Choroko		Mwinuko: 200 - 500 Mvua: 800-1,000 Joto:12-35 Udongo: pH 5-7 tifutifu, kichanga na mfinyanzi	Soya, Ufuta na nazi	Mpunga
		Nanyumbu	Korosho, karanga, njugumawe ufuta	Muhogo na mbaazi	Mwinuko: 200-500 Mvua: 800-1,000 Joto:12-35 Udongo: pH5-7 tifutifu, kichanga na mfinyanzi	Ufuta na nazi	Mahindi, Mpunga
		Newala	Korosho, Soya, ufuta	Mhogo na mbaazi	Mwinuko: 200-500 Mvua: 800-1000 Joto:12-35; Udongo:pH 5-7 tifutifu, kichanga na mfinyanzi	Ufuta na soya	Mahindi, Mpunga
		Tandahimba	Korosho, Ufuta	Mhogo, mtama na mbaazi	Mwinuko:200 -500M asl Mvua: 800-1000mm kwa mwaka Joto:12-35°C Udongo:pH 5-7 tifutifu, kichanga na mfinyanzi	Alizeti, soya	Mahindi, Mpunga
16	MWANZA	Buchosa	Pamba, mbaazi	Mpunga, mahindi na mhogo	Mwinuko: 800-1300 Mvua: 600-1,400 Joto 10 - 30, Udongo: pH 6.5 - 8.5 mfinyanzi mweusi na wa kichanga na tifutifu	Mazao ya bustani	Mtama, mhogo na viazi vitamu

Na.	MKOA	WILAYA	MAZAO YA KIPAUMBELE		IKOLOJIA	MAZAO MENGINE YANAYOWEZA KULIMWA	
			BIASHARA	CHAKULA		BIASHARA	CHAKULA
		Ilemela	Pamba, Kunde	Mpunga, mhogo	Mwinuko: 800-1,800 Mvua: 600-1,400 Joto 15 - 30, Udongo: pH 5 - 7 kichanga tifutifu, na mfinyanzi	Mazao ya bustani	Mtama, viazi vitamu
		Kwimba	Pamba, Dengu	Mpunga, mahindi na mhogo	Mwinuko: 1,000-1,300 Mvua: 600-1,200 Joto: 15 - 30 Udongo: pH 5 -7 mfinyanzi mweusi na tifutifu,	Mikunde	Mtama, viazi vitamu
